



BARAZA LA VETERINARI TANZANIA

UTARATIBU WA KUOMBA/KUJIANDIKISHA KUFANYA MAFUNZO ATAMIZI (INTERNSHIP) KWA WAHITIMU WA SHAHADA YA UDAKTARI WA WANYAMA (BVM), 2021.

Baraza la Veterinari Tanzania limeanza kupokea maombi kwa wahitimu wa shahada ya Udaktari wa Wanyama (Bachelor of Veterinary Medicine) kwa mwaka 2021 ili waweze kushiriki Mafunzo Atamizi kwa mujibu wa Sheria ya Veterinari (Sura 319). Hivyo Usajili huo unafanyika kwa njia ya Mtandao (Online application).

Hatua za kufuata kujisajili ili kuweza kushiriki mafunzo hayo ni kama ifuatavyo;

1. Ingia katika website ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi "www.mifugouvuvi.go.tz"
2. Baada ya hapo ingia "**Kanzidata ya Baraza la Veterinari**"
3. Baada ya hapo utapaswa kufungua akaunti yako kama ifuatavyo; User name "**intern**" na Password "**Intern123**"
4. Baada ya hapo utafuata maelekezo kama mfumo unavyoelekeza, na endapo utashindwa kuendelea na usajili kutokana na changamoto zozote usisite kuwasiliana nasi kwa;
 - **Dkt. Obed Nyasebwa 0689 825 862**
 - **Dkt. Aurelia Bundala 0754 260 229**
 - **Dkt. John Nzalamoto 0762 425 402**
 - **Dkt. George Mtinda 0752 363 681**

Na baada ya kujisajili katika mfumo wa Baraza kila Mhitimu atapaswa kujisajili katika Kitengo cha huduma za ajira (TaESA) kilichopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuweza kugharamiwa fedha ya nauli (TZS 150,000/=) kila mwezi kwa muda wote wa mwaka mmoja wa mafunzo, usajili huo utafanyika kupitia tovuti hii "www.portal.taesa.go.tz" baada ya kupata cheti cha kukubaliwa kufanya mafunzo atamizi toka Baraza la Veterinari.

Dkt. Bedan Masuruli
MSAJILI